**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**April, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu:**
**Mkuu wa Shule: 0784918561**
**:0769439979**
**Shule ya Sekondari Kiburubutu,**
**S.L.P 287.**
**Tarehe 25/04/2024.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….…………………………………………..**
**S.L.P ………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIBURUBUTU HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya **HGK/HGL**

Shule ya Sekondari Kiburubutu ipo umbali wa Kilometa 70 kutoka kituo kikuu cha mabasi Ifakara (Kibaoni). Usafiri kutoka kituo cha mabasi Ifakara (Kibaoni) kuja shuleni unapatikana kwa nauli isiyozidi shilingi 10,000/= kwa basi au noah. Kituo cha kushukia kinaitwa **KOTAKO Bodaboda** kilichopo kitongoji cha **Kiburubutu-Mngeta**,ukishuka chukua bodaboda hadi shuleni shilingi 1500/=.

Vilevile usafiri wa garimoshi (train) kutoka Ifakara hadi Mngeta unapatikana kwa Tsh. 3500/=,pia kwa wale wanaopitia Makambako kwa garimoshi nauli ni Tsh 12,000/=,washuke **stesheni ya Mngeta**. Chukua bodaboda kwa Tsh. 5000/= hadi shuleni.

Pia kwa wanafunzi wanaoanzia safari **Morogoro mjini (MAFIGA STENDI)** kwa usafiri wa basi watafika moja kwa moja na watashukia kituo cha KOTAKO **bodaboda** kitongoji cha **Kiburubutu-Mngeta**. (Nauli ya Morogoro-Mngeta ni Tsh 25,000/=).

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **01/07/2024,** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **30/06/2024** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **13/07/2024.**

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

**SARE ZA SHULE**

- Sketi mbili rangi ya bluu bahari (light blue) aje nazo mshono wa rinda box inayogusa kifundo cha mguu.
  - ✓ Rangi ya kitambaa cha sketi ya shule




- Mashati mawili meupe yasiyo bana aina ya tomato mikono mifupi yenye "collar" na mfuko kwa kila shati.
- Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi visivyo na urembo wowote vyenye kamba na viwe vya ngozi.
- Soksi nyeupe jozi mbili (2) zisizo na urembo au alama yoyote ya rangi.
- Sweta rangi ya light blue lenye V- shape shingoni lisiwe na alama yoyote ya rangi.

N.B kwa wasichana wa kiislamu wanaruhusiwa kuvaa nusu kanzu nyeupe isiyobana na hijabu.Pia ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. **SURUALI HAIRUSIWI**

**SARE YA KAZI/KUSHINDIA**

- Sketi mbili rangi ya "Dark Blue" mshono wa rinda box inayogusa kifundo cha mguu.
- Rangi ya kitambaa cha sketi ya kushindia/kazi



- T- Shirt mbili za shule zinapatikana shuleni (form six T- shirt) kwa shilingi 15,000/= kwa T-shirt moja.

**SARE YA MCHEZO**

- Raba za michezo
- Tracksuit rangi ya bluu bahari (light blue).
- Wakati wa michezo kila mwanafunzi atalazimika kuvaa sare ya michezo hivyo aje nazo
- Wanafunzi watavaa sare ya darasani wakati wa vipindi, na,sare ya kazi baada ya muda wa vipindi. Nguo za nyumbani **HAZIRUHUSIWI KABISA** hivyo asije nazo

## MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI:-

**VIFAA/MAHITAJI YA DARASANI**

- ❖ Madaftari kumi counter books quire 3.
- ❖ **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
- ❖ Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
- ❖ Scientific Calculator;
- ❖ Mathematical set
- ❖ Spring file moja.

**VIFAA VYA BWENI**

- ❖ Godoro lenye upana wa futi 2 1/2 (aje nalo)
- ❖ Shuka rangi ya PINKI  mbili (2)
- ❖ Blanketi moja
- ❖ Mto mmoja na foronya (2) za rangi ya pinki
- ❖ Chandarua cha rangi nyeupe pembe nne
- ❖ Ndoo ndogo mbili (02) za lita kumi, kandambili na vifaa vingine kama vile mswaki, dawa ya meno n,k
- ❖ Sahani,kikombe, bakuli na kijiko
- ❖ Kanga/kitenge doti moja na taulo kwa ajili ya kuogea
- ❖ Nguo za ndani za kutosha
- ❖ Night dress mbili
- ❖ Sanduku kubwa la bati (tranker) la kutosha vifaa vyako vyote
- ❖ Vitabu vya ibada kwa mujibu wa dini yako
- ❖ Koti la mvua/mwamvuli hususani kipindi cha mvua

- ❖ Bima ya afya (kwa mwanafunzi asiyekuwa na bima ya afya atalipia shilingi 5000/= CHF kwa mwaka )

**VIFAA VYA USAFI**

- ✓ Toilet/scrubing brush (01)
- ✓ Soft broom (fagio laini) (01)
- ✓ Hard broom (fagio la brashi ngumu 01)
- ✓ Rubber squeezer (fagio la kusukumia maji 01)
- ✓ Jembe 01 lenye mpini, na kwanja moja
- ✓ Dawa ya kusafishia vyoo (care line disinfectant lita 5).

**Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**MUHIMU:** Ulipaji wa michango yote ufanyike tawi lolote la Benki ya NMB
Jina la akaunti ni: **KIBURUBUTU SECONDARI SCHOOL RECCURENT**
**Akaunti namba: 21601200082**

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule nipamojana:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;


v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wotewawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**


i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII!**

**Saini ya Mkuu wa Shule** 

**Jina la Mkuu wa Shule: FELISTA I. NYULULU**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** 

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0784 918 561/0627 669 299**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0765 103 667**
- **Mwandamizi Taaluma:0659 513 831**
- **Mwandamizi Malezi: 0657 341 577**

**MUHIMU: Namba ya kuwasiliana au kutuma fedha za matumizi kwa mwanafunzi awapo shuleni ni 0657 341 577 iliyosajiliwa kwa jina la Felista Nyulululu (namba ya Matron).**

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi································································································

Nimesoma na kuelewa yote yaliyoelekezwa kwenye barua ya kujiunga na shule ninaahidi kuwa nitajifunza kwa bidii zangu zote, nitazingatia sheria za shule kama zilivyoainishwa, nitazifuata na nitakuwa na nidhamu wakati wote kwa manufaa yangu ya shule na Taifa kwa ujumla.

Endapo nitakiuka taratibu na kanuni za shule nitakuwa tayari kurudi nyumbani kumuita Mzazi/mlezi wangu

..........................................................................................

(Jina la mzazi/mlezi) au kusimamishwa masomo

**Jina………………………………………sahihi ………….. Tarehe……… ..**

## AHADI YA MZAZI/MLENZI

Mimi······························mzazi/mlezi wa································ninaahidi kushirikiana na shule wakati wote kuhakikisha kuwa mwanangu anafuata maelekezo yote na kutekeleza wajibu kwa shule na Taifa.

**Jina·············································sahihi ············.. Tarehe·········..**

**Namba ya simu ··················································**

KIBURUBUTU SEKONDARI SCHOOL,

P.O BOX 287,

**IFAKARA**

DATE…………………….

REF. No. …………………………………………

**PART A:**
To the medical Officer,
…………………………………………………

**REF:**…………………………………………………………………………………………………………….

Please examine the above – named student as to her physical and mental fitness for being student. Each defect will hinder a girl for secondary education.

1. a). Eye sight
   b) hearing
   c) Limbs
   d) Speech
   e) venereal disease
   f) Leprosy
   g) Epilepsy
2. neurosis
3. other serious diseases
4. pregnancy

**PART B: MEDICAL CERTFICATE**

(To be completed by a GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)

I have examined the above – named student and confirm that she is physically fit/ not fit for a full time secondary school Education.

a. Eye sight ………………………………………………..
b. Hearing …………………………………………………..
c. Limbs ……………………………………………………..
d. Speech …………………………………………….
e. Venereal diseases ………………………………..

f. Leprosy …………………………………
g. Epilepsy ………………………………
h. Neurosis………………………………
i. Other serious diseases …………………
j. Pregnancy ………………………………….

Name ……………………………………………………………… Signature ……………………………Date ……………………………

STATION …………………………………………………………………..

DESIGNATION ………………………………………………………

NB: I request this form to be returned to the school in a sealed envelope.

## FOMU ZA HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………………..
2. JINA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI …………………………………
3. JINA LA SHULE ANAKOTOKA ……………………………………..
4. TAREHE YA KUZALIWA …………………………
5. KATA ANAYOTOKA MWANAFUNZI…………………………….…………
6. WILAYA ANAYOTOKA MWANAFUNZI …………………………………
7. MKOA ANAOTOKA MWANAFUNZI……………………………………..
8. KABILA……………………………………………………
9. URAIA ……………………………………………………..
10. DINI/DHEHEBU ………………………………………
11. ANUANI YA MZAZI/MLEZI …………………………
12. NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI NYUMBANI ………………………

OFISINI ………………………………………………………………………….

E- MAIL ADRESS ………………………………………

ANUANI YA POSTA KWA AJILI YA KUTUMA MATOKEO YA MTIHANI:-

………………………………………………………………………………………

13. MAJINA MANNE YA NDUGU WA KARIBU WALIOIDHINISHWA KUCHUKUA NAFASI YA MZAZI/MLEZI ENDAPO DHARURA ITATOKEA;-

| Na | JINA | UHUSIANO | ANAKOISHI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |

**KIBURUBUTU SEKONDARI SCHOOL**
**A – LEVEL BOOKS REQUIREMENTS**

**GEOGRAPHY PARER 1**

1. Principles of physical Geography – by F.J Monkhouse
2. A comprehensive approach to physical Geography for secondary school – by D.T Msabila
3. Practical Geography for Africa By John M. Prichard
4. Land forms in Africa – an introduction to Geomorphology – by Colin Buckle
5. Africa – by J.M Prichard
6. Practical Geography for A level – by Francis Mnyawi
7. An integrated approach to Geography – by David Waugh

**GEOGRAPHY PAPER II.**

1. Human and Economic Geography – by Goh Cheng & Morgan
2. Advanced level geography Course book – by Tanzania Institute of Education (TIE)
3. An integrated focal regional study on human and Economic Geography Advanced level paper 2 – by D. T Msabila

**ENGLSH LANGUAGE**

1. A practical approach by Asheli, N.E
2. An introduction to Language Advanced level by. Kadeghe, M

**ENGLISH LANGUAGE 2**

**NOVELS AND SHORT STORIES**

1. A man of the people by Chinua Achebe
2. The beautiful ones are not yet Born by. Ayi Ewei Armah
3. His Excellency the head of state by Sago

**B: PLAYS**

1. I will marry when I want by Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Murrii
2. An enemy of the people by. H.Ibsen
3. The Causasian Chalk Circle by. B.Bretch
4. Betrayal in the City by. F.Imbuga
5. Not yet Uhuru
6. Rwanda Magere

7. Black Mamba

C. **POETRY:**

1. Tanzania institute of Education: selected poems
2. David Cook et. Al: poems from East Africa

**HISTORY:**

(i) How Europe underdeveloped Africa: Nairobi Heinemann Kenya (1992) by. Rodney W

(ii) Africa in world History A- Level Certificate Notes DSM (DUP) 1992. By Nyirenda H. D

(iii) Essays on the theory and practictice of imperialism DSM, THP (1979) by. Nabudere D.W

(iv) Imperialism the Highest stage of capitalism Moscow, Progress Publishers by Lennin, V.I.(1982)

(v) Advanced level – History Notes, Selected Topics for paper 1&2 (2002) by Nyangwine, N

(vi) Major events in African History (2015) by. Fr Jovitus F. Kimara Mwijage

**KISWAHILI 1.**

1. Historia ya kiswahili by Mbunda
2. Educational Publishers and distributors Ltd, Dar Es Salaam by, Msokile (1992)
3. Kiswahili sekondari by, Taasisi ya ukuzaji mitaala (1958)
4. DUP by. James s. mdee (1988)
5. Kiswahili kidato cha tano na sita by, Oxford University press (2012)

**KISWAHILI 2**

1. Fasihi by. Senkoro, F.E.M.K (2011)
2. Macmillan AIDAN, DSM by Morani, Emmanuel Mboga.
3. Kwenye ukingo wa THim. By. Ebrahim Hussein

**Riwaya**

1. Kufikirika shaaban Robert. Mkuki na nyota Publishers. Dar Es Salaam, (2003)
2. Mfadhili Hussein Tuwa Macmillan Aidan, (2007)
3. Usik utakapokwisha. Mbunda Msokile, Macmillan
4. Vuta Nkuvute. Shafi A. Ahafi, Mkuki na nyota Punlishers, DSM (1999)

**Tamthiliya**

1. Nguzo mama. Pennina mhando. Macmililan AIDAN,DSM (2007)
2. Kivuli kinaishi Said A. Mohamed Oxford University Press
3. Morani. Emmanuel Mbogo. Macmillan AIDAN, DSM

**Ushairi**

1. Mapenzi bora saaban Robert. Mkuki na Nyota Publishers (2007)
2. Chungu tamu T.A Mvungi THP DSM, (2000)
3. Fungate ya Uhuru. Mohamed SEif Khatib, DUP, DSM,(2000)
4. Kimbunga. Haji Gora haji. TUKI,DSM (2003).